# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P 02,
**USHIROMBO**
*BUKOMBE*

***MKOA WA GEITA:***
***Simu:*** *028 2520709*
ded@bukombedc.go.tz

# TANGAZO KWA WANANCHI WOTE BUKOMBE

**Kumekuwepo na uvumi kuhusu hatari dhidi ya Buu/Pupae wa vipepeo jamii ya *Spalgis* ambao hutokea mara chache katika mazingira yetu hasa kipindi cha Kiangazi na jamii imewaita "Kidudu mtu" kwamba, wameonekana kwenye mazao ya mbogamboga na matunda na wanamadhara makubwa kiafya kwa kusababisha mauti pindi mboga hizo zinapotumika kwa chakula.**

**Uvumi huu umesababababisha hofu kubwa kwa wananchi ambao ni watumiaji wa mboga za majani na matunda, na kupelekea biashara ya mbogamboga kuathirika kwa baadhi ya maeneo hapa wilayani.**

**Kupitia tangazo hili, ifahamike kwamba chanzo cha kuwepo kwa "kidudu mtu" kwenye mazao yakiwemo ya mbogamboga na matunda ni kutokana na kuwepo kwa wadudu wengine waitwao *VIDUNGATA/MEALBUGS* ambao hushambulia mazao mbalimbali kama vile; Mihogo,Mipapai, Mbaazi, Nyanya, Pamba, na mipera.**
**Hivyo, wananchi mnataarifiwa kidudu mtu ni wadudu rafiki kwa mkulima kwani wapo kwenye mazao kwa ajili ya kuwashambulia Vidungata ambao ni wadudu adui kwa mkulima kwa hali hiyo,kidudu mtu hawana madhara kwa watumiaji wa matunda na mboga mboga.**

**Aidha, ifahamike kwamba wadudu hao waliobatizwa kwa jina la vidudu mtu kutokana na mwonekano wao ni vipepeo na ni hatua moja wapo ya ukuaji wa wadudu vipepeo.**

**Ikumbukwe kwamba, kwa wadudu Kamili katika ukuaji wanapitia hatua nne zifuatazo hadi kukamilika, hatua hizo ni;**

**Yai → Funza → Buu → Mdudu Kamili**





C

**Hivyo basi, kutokana na ukweli huu, ushauri kwa wananchi ni kuendelea kutumia mbogamboga kwani hakuna Madhara yoyote Mwananchi atakayopata.**

**Wakulima,wafanyabiashara na walaji wa mbogamboga na matunda wasafishe mazao yao yaliyo na wadudu hao kabla ya kuyatumia ili kuepusha fikra potofu zilizoenea za madhara ya wadudu hawa na hivyo kusababisha hofu ya kutumia mbogamboga na matunda ambavyo ni mojawapo ya vyanzo vya lishe muhimu kwa binadamu na kipato kwa wakulima na wafanyabiashara wa mboga na matunda.**

**Imetolewa na;**
**Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Bukombe.**
**21/06/2017.**